**Pendekezo la mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu hatari za madini ya mercury, yaani zebaki kwa Baraza Kuu la UNEP katika mkutano wa Januari, 2007**

**Maelezo Maalum**

Madini ya zebaki yana sumu kali mno. Sumu hiyo inaweza kusababisha madhara kwa uti wa mgongo hata yakiwepo katika viwango vidogo sana. Sumu hii hupatikana kwenye vyakula, hasa samaki na pia hupatikana katika miili ya binadamu na wanyama, na huathiri vibaya zaidi watoto kabla hawajazaliwa na wakiwa wachanga. Madini haya husafiri masafa marefu hewani katika nchi mbalimbali na yameathiri vyakula kote ulimwenguni na kuzua hatari kubwa.

Kwa vile hatua ambazo zimechukuliwa kufikia sasa hazijapunguza hatari ya madini haya (tazama jedwali 1 na 2 hapo chini), pana haja ya kuchukua hatua maalum kwenye viwango vya kimataifa kwa njia nyingi zikiwemo njia zifuatazo:

**1.** Hatua zinapaswa kuchukuliwa haraka iwezekanavyo ili kufikia makubaliano rasmi kuhusu madini ya zebaki kwenye ngazi za kimataifa.

**2.** Kutetekelezwa kwa mapendekezo yaliyotolewa kwa Baraza Kuu la UNEP na hatua kuchukuliwa kama ifuatavyo:

**3.** Kupunguza matumizi ya madini ya zebaki kote ulimwenguni

a) Mpango rasmi wa kupunguza matumizi ya madini hatari ya zebaki ulimwenguni kwa asilimia 50% kufikia 2012 na kwa 70% kufikia 2017 ikilinganishwa na mwaka wa 2005 lazima uanzishwe (tazama jedwali muafaka)

b) Mbinu za kupunguza zebaki zinaopaswa kutekelezwa kwa njia hizi:

i) Kupitishwa kwa sheria ya kupiga marufuku matumizi ya madini hatari kwenye utengenezaji wa **vifaa vya stima na vingine vinavyotegemea umeme** katika nchi zote zinazounda vifaa hivyo;

ii) Kupiga marufuku matumizi ya zebaki katika utengenezaji wa betri - za magari na za tochi

iii) Kukomesha matumizi ya vifaa vya kupima joto mwilini (*thermometers*) vinayotengenezwa kwa zebaki na kupunguza uundaji wa **vifaa vyoyote vya kupimia visivyotegemea stima lakini vinavyotumia zebaki.** Taasisi za kimataifa, serikali, hospitali na mashirika mengine makubwa yanayonunua vifaa vya matibabu yanapaswa kusaidia kuhakikisha yanatumia vipima-joto ambavyo havijaundwa kutumia zebaki; kadhalika, mashirika yaunge mkono sheria zozote za kupinga utumizi wa zebaki;

iv) Kuhakikisha kuwa **bidhaa zenye zebaki na mikakati yoyote inayotumia zebaki** katika mataifa yaliyostawi kiviwanda haipelekwi katika mataifa ambayo hayajastawi;

v) Kukomesha matumizi ya betri za zebaki na vifaa vya chlor-alkali vinavyotegemea zebaki haraka iwezekanavyo. Ili kutekeleza mabadiliko haya, mpango maalum wa kusaidia kifedha mataifa yasiyostawi unapaswa kutekelezwa na UNEP uwe tayari kufikia wakati wa mkutano maalum wa Baraza Kuu lake utakaofanyika 2009.

vi) Kuanzisha mpango maalum kwa wachimbaji dhahabu wa viwango vidogo unaolenga kila sekta inayohusika – wenye madhumuni ya kupunguza matumizi ya zebaki kwa asilimia 50% kufikia 2017 kama ilivyopendekezwa na Mradi Maalum wa Zebaki wa shirika la UNIDO, ambao unaweza tu kufanikiwa kwa kukomesha matumizi ya zebaki katika utengenezaji wa chuma, na kutumia mbinu zingine zozote kwa kushirikiana na mataifa mengine kutekeleza mikakati ya kupunguza matumizi ya zebaki katika sekta ya uchimbaji.

**4.** Kupunguza mioshi ya zebaki ulimwenguni

UNEP inapaswa kuandaa taarifa rasmi kuhusu madhara ya mioshi yenye zebaki na pia kutoa mapendekezo kuhusu jinsi za kupunguza mioshi hiyo kwa vipindi vya miaka 5 au 10 ijayo. Mapendekezo hayo yanafaa kujadiliwa kwenye mkutano wa 25 wa baraza Kuu la UNEP utakaofanyika 2009. Mapendekezo hayo yanapaswa kujadili hasa sehemu masuala ambayo yamepuuzwa kwenye mijadala ya

awali kuhusu mbinu za kupunguza hatari zinazotokana na zebaki. Haja kuu ni kupunguza hatari zote kutokana na mioshi ya zebaki."

**5.** Kupunguza Mauzo ya Zebaki Ulimwenguni

a.) Mkusanyiko wa wanaouza zebaki kwa matumizi ya biashara unapaswa kuandaliwa rasmi ili kutekeleza matumizi ya mabaki yoyote yanayotokana na matumizi ya zebaki ili kuyapunguza kwa jumla kuanzia kwenye miradi ya kuchimba madini hayo hatari hadi kwenye viwanda vinavyohusika. Uchimbaji wa madini ndio hasa unaotegemea matumizi ya zebaki zaidi kwani huongeza kiwango cha zebaki na kufuka mioshi hatari kwa viumbe.

b.) Uuzaji wa zebaki kwa wingi unapaswa kuzuiwa kwenye soko za kimataifa kwa njia zifuatazo:

i. **Kupunguza mauzo ya zebaki nje** ya mataifa yaliyostawi
ii. Kuorodhesha zebaki kwenye Makubaliano Rasmi ya Rotterdam yanayosisitiza **Makubaliano ya Awali** kabla ya mabaki ya zebaki kusafirishwa popote
iii. **Kutekeleza miradi tofauti ya kisasa** isiyotegemea zebaki itakayochukua mahali pa uchimbaji ambapo zebaki imekuwa ikitumika; na
iv. Kuanzisha jopo maalum la kutoa mapendekezo ya kuelekeza ukomeshaji wa biashara zinazotumia zebaki na *chlor-alkali* kupitia kwa usimamizi wa viwanda vyake vinavyofungwa.

**6.** Usaidizi wa kifedha

Mataifa yaliyostawi yanapaswa kutoa pesa zaidi za kughramia miradi hii katika mataifa yanayopiga hatua kimaendeleo, na GEF pamoja na taasisi zingine zinapaswa kuanzisha mradi wa kifedha wa kutoa usaidizi kutekeleza mbinu za kupunguza matumizi ya zebaki kwa misingi ya mapendekezo yaliyotajwa.

## KUMBUKA: MATUMIZI YA ZEBAKI ULIMWENGUNI NA MAPENDEKEZO TANGU MIAKA YA 1990 – HATUA DUNI MNO

Jedwali 1 limeandaliwa kutokana na ripoti iliyochapishwa majuzi ya biashara ya zebaki. Ripoti yenyewe iliandaliwa Baraza Kuu la UNEP na inaonyesha kuwa matumizi ya zebaki ulimwenguni hayajabadilika mno tangu 1994 huku mataifa yaliyostawi yakuelekeza zebaki na teknolojia za zamani kwenye mataifa yanayopiga hatua kimaendeleo. Jedwali2 limeandaliwa kwenye misingi ya kazi ya Jozef Pacyna na washirika wake na inaonyesha kwamba viwango vya zebaki angani vimeongezeka kutokana na asili kama uchomaji makaa, uteketezaji wa bidhaa za vyuma viwandani hasa *zinc* na shaba), viwanda vya chlor-alkali na utupaji takataka zozote zenye mabaki ya zebaki.






**Hali ya mahitaji ya zebaki**

| Sekta | 2005 | 2012 | 2017 | Maoni – Mbinu za kupunguza |
|---|---|---|---|---|
| Betri | 400 | 50 | 25 | Kupunguza ulimwenguni betri za zebaki |
| Chlor-alkali | 620 (535 net) | 300 | 0 | Kumaliza ulimwenguni kufikia 2015; Mkutano wa India unaazimia kumaliza kufikia 2012 |
| Vifaa vya kupima | 250 | 75 | 50 | State action achieves tipping point in USA; EU and China prohibit sale |
| Swichi/Vibonye | 250 | 50 | 50 | Maelekezo ya Jumuiya ya Ulaya na Uchina na EU (RoHS) ; uamuzi wa serikali Amerika wakaribia kutekelezwa |
| Umeme | 120 | 150 | 110 | Matumizi ya taa za umeme huongezeka zaidi katika miaka 5, kasha mbinu zingine huibuka |
| Kwa meno | 270 | 135 | 75 | Matumizi kwenye shughuli za kutunza meno hupunguka kutegemea mbinu za kisasa na hatua za kisheria |
| Uchimbaji dhahabu kwa viwango vidogo | 800-1,000 | 600 | 400 | Hatua za kimataifa za kukomesha matumizi ya zebaki kwenye viwanda vya vyuma na mbinu zingine za kupunguza matumizi ya zebaki: tazama ripoti ya UNIDO kwa UNEP |
| PVC | 700 (350 net) | 550 | 300 | Matumizi zaidi nchini Uchina; njia zitafutwe za kupunguza matumizi kisha hatua zichukuliwe kupiga marufuku; hatua kuhusu mbinu tofauti za kuepuka zebaki zitekelezwe katika kipindi cha miaka 10. |
| Zingine | 50 | 25 | 10 | Chanjo/rangi, n.k. |
| Jumla | 3,460 to 3,660 | 1,885 | 1,020 | Hatua maalum za kuwezesha kupunguza zebaki katika miaka 10 ijayo ni: Piga marufuku matumizi ya zebaki kutengeneza betri nchini Uchina, Jumuiya ya Ulaya na Japan; Piga marufuku matumizxi ya vifaa vya kupima vya zebaki katika Jumuiya ya Ulaya na Uchina; mafanikio kwenye upunguzaji wa uundaji wa betri za zebaki ; matumizi bora zaidi ya nchini Uchina; kupunguza mauzo ya zebaki na kuongeza bei ya ASM; kukomesha matumizi ya bidhaa za vyuma katika ASM |

[1] Kundi la **Zero Mercury Working Group**, www.zeromercury.org, ni mkusanyiko wa kimataifa wenye mashirika zaidi ya 48 ulioanzishwa 2005 na mashirika ya European Environmental Bureau na Mercury Policy Project/Ban Mercury Working Group. Lengo maalum la mashirika haya ni kufikia hali ambapo hakutakuwa na mioshi ya kuharibu hewa, kukomesha mauzo na mahitaji ya zebaki katika nyanja zote iwezekanavyo hadi kumaliza zebaki kabisa kwenye mazingira kufikia kiwango cha Jumuiya ya Ulaya na kwingneko kote ulimwenguni.